

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي
مشروع تعلم الإسلام - أحكام الصلاة - سواحيلي

Samo la 7

الدرس السابع

MAMBO YA WAJIBU KWENYE SWALA.

1. Takbira zote isipokuwa takbira ya kuhirimia swala.
2. Kusema SIUBHANA RABBIYAL ADHWIMU mara moja.
3. Kusema SIMI'ALLAHU LIMAN HAMIDA kwa Imam na kwa mtu pekee, wakati wa kunyanyuka kutoka kurukuu.
4. Kusema RABBANA WALAKAL HAMDU bada ya kutoka kurukuu.
5. Kusema SUBHANA RABBIYAL A'ALA mara moja katika kusujudu.
6. Kusema RABBIGHFIRILII kati ya sijda mbili.
7. Tahiyyatu ya kwanza.
8. Kikao cha tahiyyatu ya kwanza.

NGUZO ZA SWALA.

1. Kusimama pamoja na uwezo kwenye swala za faradhi, kwa swala za sunnah sio lazima kusimama, lakini kuswali kwa kukaa ina ujira wa nusu kuliko yule mwenye kuswali kusimama
2. Takbira ya kuhirimia swala.
3. Kusoma surat fatiha katika kila rakaa.
4. Kurukuu kwa kila rakaa.
5. Kuitadili kutoka kurukuu kwa kusimama wima.
6. Kusujudi kwa viungo saba mara mbili kwa kila rakaa.
7. Kukaa kati ya sijda mbili.
8. Kujituliza katika vitendo vyote tulivyo vitaja hapo juu.
9. Tahiyyatu ya mwisho.
10. Kitako cha tahiyyatu ya mwisho.
11. Kumswalia Mtume (saw)
- 12 . Kutoa salamu.
- 13 . kufuata mpangilio kwa kila nguzo.